

KUONDOKA GHAFLA

KWA KANISA, KWA SIRI

 Inapasa kumfanya mtu yeyote ajisikie vizuri, sivyo, utangulizi kama huo? Vema. Hebu na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda mfupi tu wa maombi kabla hatujalifungua Neno.

² Bwana, tunasema kama watu wa kale, “Nilifurahi waliposema, ‘Twendeni Nyumbani kwa Bwana.’” Hatuwezi kupata mahali pazuri zaidi pa kuwapo, leo, kuliko kuwa papa hapa pamoja na kusanyiko la Bwana, katika ibada. Ingawa huenda inanyesha, huko nje, na kunaweza kuwa na taabu na kadhalika, lakini tunapokuwa katika Uwepo Wako, tuna tabasamu hili la kuridhika, kwamba tunajua kwamba Wewe unaelewa na unafanya kila kitu vyema kabisa kwa ajili yetu.

³ Tungeomba baraka maalum asubuhi ya leo kwa ajili ya wale ambao hawakuweza kufika kwenye ibada. Wengi, labda, wangekuja kama hali ya hewa haikuwa mbaya hivi. Lakini na wapate faraja kwa kusoma Neno Lako, na kuwasikiliza wahudumu kwenye redio, na vipindi ambavyo vimetayarishwa kwa ajili ya watu hao.

⁴ Tungeomba kwamba ungewabariki hasa wale walio katika Uwepo wa Kiungu, kwa ajili ya juhudi zao za kuja asubuhi ya leo, kusikia Neno la Bwana, na kumtumikia katika Zaburi na katika—katika maombi, na katika shukrani.

⁵ Pia tunaomba, Mungu, kwamba utaigusa miili ya walio wagonjwa na wahitaji, ambao wanangoja sasa hivi, wamekuja kutoka mbali wapate kuombewa.

⁶ Basi tunaomba ya kwamba Wewe utuangelie tu, na unene nasi, ili kwamba sisi tulio hapa asubuhi ya leo tuchunguze hali yetu wenyewe, “Nichunguze,” alisema mmoja wa manabii, “na unijaribu, uone kama kuna uovu wowote ndani yangu.” Ndipo basi, Bwana, katika kuchunguza, ukiona kwamba kuna uovu ndani yetu, ututakase, Bwana, tunapoungama kwa unyenyekevu dhambi zetu na matendo yetu maovu.

⁷ Nasi tunaomba tu kwamba utukumbuke unapomtazama Yesu, Mwanao, Ambaye alikufa apate kuwa upatanisho kwa ajili ya dhambi zetu na uovu wetu. Tunapokiri kwamba tunaamini kwamba alikufa kwa kusudi hili, na kufufuka tena, kwamba tungekuwa na majaliwa makuu ya kufanya jambo hili, asubuhi ya leo. Tujalie, Bwana.

⁸ Na unene nasi kupitia Neno Lako lililoandikwa, tunapongojea zaidi kusikia kutoka Kwako. Katika Jina la Yesu tunaomba. Amina.

⁹ Tunataka kufungua Maandiko asubuhi ya leo tupate kusoma katika Kitabu cha Wathesalonike, mlango wa 5. Nami ninao wale walio na haja ya maombi pia, asubuhi ya leo, ile orodha. Ambapo, maombi yatatolewa mara tu baada ya ibada hii ya kuhubiri. Ninaamini, kwa muda mfupi tu, kwenu ninyi mnaofungua Biblia zenu, hebu tufungue Wathesalonike wa Kwanza mlango wa 5, na tusome kwa dakika chache tu.

¹⁰ [Ndugu mmoja anasema, “Ruhusu madarasa ya shule ya Jumapili waondoke.”—Mh.] Samahani. Wakati ukifungua Biblia yako, ni . . . watoto bado hawajaruhusiwa kwenda kwenye madarasa yao mbalimbali. Naomba mwende sasa hivi kwenye madarasa yenu, ninyi watoto wadogo na matineja, na kadhalika. Nendeni moja kwa moja kwenye madarasa yenu.

¹¹ Na wakati, kama mnaweza sasa, kusoma, au kufungua Biblia zenu kwenye Wathesalonike wa Kwanza mlango wa 5.

¹² Na kama inawezekana kwamba halmashauri ya wadhamini ipo wakati huo, ningependa kuwaona dakika chache tu baada ya ibada, katika ofisi ya mashemasi, kuhusu shughuli fulani. Na kama hawako, mtu fulani awapashe habari kwamba ningependa kuwaona usiku wa leo, kabla tu ya ibada, katika ofisi ya mashemasi.

¹³ Sasa kwa ajili ya somo, ninataka kuchukua hili kama somo asubuhi ya leo: *Kuondoka Ghafla Kwa Kanisa, Kwa Siri.*

¹⁴ Hebu mimi . . . hebu nilitangaze tena, kwa sababu sijawa na wakati mwingi wa kutafakari juu ya mafafanuzi yoyote, lakini niliharakisha tu. Tulichelewa huko nje jana jioni, wala sikurudi jana usiku hadi usiku sana. Kisha nikaharakisha kuja hapa asubuhi ya leo, lakini hili limenijia hivi punde tu mawazoni. Na labda, baadaye, ninaweza kupata kitu ambacho kingemfaidi mtu fulani. Ninapenda somo hili, “Kunyakuliwa ghafla kwa Kanisa kwa siri.” Na sasa katika Wathesalonike wa Kwanza mlango wa 5.

Lakini, ndugu, kwa habari ya nyakati na majira, hamna haja niwaandikie.

Maana ninyi wenyewe mnajua yakini ya kuwa siku ya Bwana yaja kama vile mwivi ajavyo usiku.

Maana watakaposema, Amani na salama; ndipo maangamizi ya ghafla yatakapowajilia, kama vile utungu umjiavyo mwanamke mwenye mimba; wala hakika hawataokolewa.

Lakini ninyi, ndugu, hamumo gizani, hata siku hiyo iwapate kama mwivi.

Ninyi ni . . . wana wa nuru, na wana wa mchana: sisi si wa usiku, wala wa giza.

Basi tusilale usingizi kama wengine; bali tukeshe na kuwa na kiasi.

Kwa maana walalao hulala usiku; na walewao hulewa usiku.

¹⁵ Sasa nawatakeni mwangalie tu upande huo mwingine wa ukurasa, kama umepangwa kijiografia namna hiyo kabisa katika Biblia yako, kwenye vifungu vya 16, 17 na 18 vya mlango wa 4 wa Wathesalonike wa Kwanza.

Kwa maana Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni pamoja na mwaliko, na sauti ya malaika mkuu, na parapanda ya Mungu: nao waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza:

Kisha sisi tulio hai, tuliosalia, tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu, ili tumlaki Bwana hewani: na hivyo tutakuwa pamoja na Bwana milele.

Basi farijianeni kwa maneno haya.

¹⁶ Bwana na aongeze baraka Zake kwenye kusomwa kwa Neno Lake takatifu.

¹⁷ Hili ni jambo lisilo la kawaida, kuzungumza juu ya somo kama hili asubuhi niliyoshuka kuja ku—kuwahudumia wagonjwa. Lakini kuna ugonjwa mkubwa zaidi kuliko ugonjwa wa mwili. Na ni muhimu zaidi sana kwamba tuwe wazima, kwa ajili ya tukio hili kuu ambalo linakaribia kutukia, kuliko vile ingekuwa tukilala katika Bwana, yaani, kufa, kama vile tungelijua. Ni bora zaidi kuwa tayari. Afadhali niwe mgonjwa, nikiwa tayari pamoja na Bwana, kuliko kuwa mwenye afya, asiye tayari kwenda pamoja na Bwana. Lakini vyovyote vile, Mungu anapenda sana kwamba tuwe wazima na tayari, nafsi na mwili. “Maana Yeye hutusamehe maovu yetu yote, na kuponya magonjwa yetu yote.” Alikufa kwa kusudi maradufu.

¹⁸ Halafu basi, ninawazia leo juu ya somo hili la, “Kwa ghafla, na kwa siri.” Napenda hilo. Mungu. . .

¹⁹ Watu wanaishi siku hizi kana kwamba, ni kabla tu ya Kuja kwa Bwana Yesu, kama kwamba atatuma jeshi la Malaika kwenye magazeti yote, na, kwa mwaka mmoja au zaidi, watangaze kote ulimwenguni, kwenye gazeti, kwamba, “Mnamo tarehe *fulani-fulani*, Yesu atawasili.” Na kukutangaza kwa radio, na kuwekwa kwenye televisheni, na kila mahali, siku hasa na saa yenyewe ambayo Yeye anakuja. Sasa hivyo ndivyo watu wanavyoishi siku hizi.

²⁰ Lakini, Mungu amesema katika Neno Lake, ya kwamba, “Itakuwa kama mwivi usiku, akija.”

²¹ Kama ingekuwa hivyo, watu wangesema, kama ulimwengu unavyofikiria siku hizi, “Loo, vema, kuna muda mwingi tu. Nitaninii... Itatangazwa vyema.” Na, lakini, mnaona, inatangazwa, lakini ni tangazo la kisiri. Ni wale tu walio tayari kusikia. Wale ambao wako tayari kulizingatia na... wanaompenda Bwana.

²² Sasa nawazia kile Paulo alichosema aliposema, “Nimewekewa taji ya haki, ambayo Bwana, Mwamuzi wa haki atanipa siku hiyo.” Kisha akasimama. Je, mlima? Kisha akasema, “Si mimi tu, bali na wale wote wanaompenda kuonekana Kwake.” Iwapo tunapenda kuonekana Kwake!

²³ Kwa kawaida ulimwenguni siku hizi, ni kwamba watu huwazia kuonekana kwa Bwana kama jambo la kutisha, la kuogofya. Loo, ulimwengu unaweza ukafikia ninii yake... “Usinzungumzie kuhusu hilo,” watasema. Hawataki kujua kuhusu mambo hayo. Hawayajali; ila tu maisha ya sasa. Lakini wale wanaompenda Bwana, wanapenda kuonekana Kwake.

²⁴ Vipi kama mmoja wa wapendwa wako, baadhi yenu watu wazima, kwamba mama yako amekuacha, au baba yako, au mtoto wako mchanga, nao wameondoka kwa miaka mingi sana, nawe ulijua ya kwamba huenda wakatokea wakati wowote? Mbona, ungeifagia sana nyumba. Ungekuwa tayari tu na kuitazama barabara hiyo, kwa kuwa, kila taa ya gari linaloingia, ungefikiri ingekuwa ni wao.

²⁵ Sasa hivyo ndivyo Kanisa linapaswa kuwa likikutarajia Kuja kwa Bwana. Yote katika utaratibu, yote tayari, yote yamepakiwa na tayari kwenda mara tu Yeye ajapo, kwa sababu, “Itakuwa katika dakika moja, kufumba na kufumbua jicho.” Jaribu tu kupima ingechukua jicho lako muda gani kufumba na kufumbua, hivyo ndivyo tu Unyakuo wa Kanisa utakavyotukia haraka.

²⁶ Unajua, adui sikuzote hutumia mbinu ambazo—ambazo Bwana hutumia. Mnajua, alipoona ya kwamba Mungu alikuwa anaenda kuwa na Kanisa lenye haki, na mambo ambayo Yeye angefanya, adui alitumia mbinu iyo hiyo. Yeye ana kanisa, tena ana watu ambao ni wa kidini sana. Nao wako macho kabisa, kama—kama watu wa kidini, kwa sababu anajua kwamba Kanisa la Kristo ni vivyo hivyo.

²⁷ Naye anafanya hivyo katika maisha ya kijeshi. Nilikuwa nikisoma makala siku moja, juu ya lile shambulizi la ghafla la Bandari ya Pearl. Hilo halikuwa hasa, shambulio lolote lisilojulikana. Tayari walikuwa wameonywa kwamba Wajapani wangepanya hivyo. Lakini jambo la kusikitisha ni kwamba, walipuuza onyo hilo. Walikuwa wameona dalili, na jeshi la Wajapani likikusanyika pamoja, na manowari kubwa zikiwa zimepakiwa makambora, nalo tishio lilikuwa hewani. Nao

walikuwa kabisa kwenye mstari wa huo uvamizi, lakini wakaupuuza.

²⁸ Hivyo ndivyo ilivyo siku hizi kwa kanisa. Kanisa liko kwenye mstari wa hukumu, lakini wanapuuza Kuja kwa Bwana. Hata huwezi kumlaumu Yeye.

²⁹ Walisema, ilipotangazwa, kote, katika Bandari ya Pearl, kwamba Wajapani wangeweza kushambulia wakati wowote, na kwamba kundi lao kubwa la manowari lilikuwa limeingia kwenye maji ya bahari na lilikuwa likisonga mbele polepole lakini kwa uthabiti kuelekea Bandari ya Pearl, kwamba walicheka tu. Na kusema, “Aha, upuuzi. Enyi waleta huzuni. Enyi wenye wasiwasi usio na maana. Yote mnayowazia ni matatizo tu.”

³⁰ Basi huo usiku, kabla tu ya lile shambulizi kuu kesho yake asubuhi, kulikuwa na dansi kubwa, au karamu kubwa iliyoandaliwa katika Bandari ya Pearl yenyewe. Na haijalishi ni kiasi gani walijaribu kusema kwamba Wajapani walikuwa wanakuja, bado hawangepokea onyo.

³¹ Hebu tuwaangalie tu kwa dakika chache. Kuna taarifa ndogo rasmi ya redio inayotolewa. Na kipande kidogo pembeni mwa gazeti, kama vile uamsho wa uponyaji ungetangazwa, sehemu ndogo tu, kwamba Wajapani walikuwa njiani wakija katika maji ya bahari, kundi kubwa la manowari lilikuwa linaelekea huko. “Upuuzi,” wanasema wengine. “Hatuamini katika upuuzi kama huo. Mnajaribu kututishia nini?”

³² Ndipo basi tunaona, ikikaribia usiku, ninaweza kuona nyumbani, badala ya wao kujiandaa kutoka nje ya jiji, mbona, wasichana wadogo wote walikuwa wanavaa nguo zao mpya, na kadhalika. Walikuwa wakishuka kwenye yubile hii kubwa sana waliyokuwa wanaenda kuwa nayo.

³³ Na, pia, maafisa wa Jeshi walikuwa na shughuli nyingi tu wakiandika pasi ndogondogo kusudi askari wote wahudhurie karamu hii, karamu kubwa ya ulevi. Nayo malori yalikuwa yakinguruma na kuvuma, yakileta bia zao bora kabisa, na divai yao na kadhalika, kwa ajili ya karamu hii. Na wakati wote, kundi la manowari za Kijapani ziko njiani kule, nao wanakosa kusikia onyo.

³⁴ Basi jua lilipoanza kutua, nao wote wakakusanyika katika sehemu hii kubwa ya vilabu vya pombe. Labda kando mahali fulani, mhudumu wa baa akiing’arisha baa ama chochote kile, alisema kitu kama hiki, “Aise, umesikia uvumi huo?”

“Hapana, siamini niliusikia,” alisema mtu aliyezungumza naye.

³⁵ “Loo, wanasema jambo kuhusu manowari za Kijapani kuja huku.” Halafu mtu mwingine anaingilia hayo mazungumzo.

36 Naye msichana mdogo, mpumbavu anaruka pale, na kuweka mguu wake kwenye ukingo, kasema, “Ninyi majipu yenye vichwa vilivyojaa huzuni, hamjui kwamba tuko hapa kwa ajili ya kula raha wala si kupayuka-payuka kuhusu vita?”

37 Ikiwa hivyo sivyo karibu tu ulimwengu unavyosema siku hizi kuhusu Kuja kwa Bwana! “Ewe wa mtindo wa kale usiyelewa, wa kizamani, ni nini kinachokufanya uvae na kufanya na kutenda vile unavyotenda?” Lakini tunakutazamia huko kuonekana ghafla kwa Bwana, kwa siri. Kwa maana kuna kitu fulani hewani, Ujumbe wa Roho Mtakatifu, unaotuambia kule Kuja kumekaribia.

38 Ndipo wakati zile shamrashamra kubwa zilipoendelea, na, loo, hapana shaka lilikuwa ni jambo la kutisha usiku huo. Kwa maana ilisema kwamba wakati fulani usiku, walimchukua msichana, msichana mwenye sura nzuri aliyeumbika, nao wakamvua nguo zake, na kumweka ndani ya mkokoteni mdogo akiwa na vazi moja tu la ndani, na kumpitisha mtaani na kadhalika, wakiwa tu na wakati mzuri. Na wakati huo wote, Wajapani walikuwa wakipiga hatua, wakija moja kwa moja.

39 Na ndipo kesho yake asubuhi, wakati watu walioshika zamu, na waangalizi wa selo za ndege, na kadhalika, walikuwa nje usiku kucha, wamelewa, na kuzurura na wanawake hawa na kadhalika, walikuwa na usingizi na fadhaa asubuhi iliyofuata, kutoka kwenye karamu kubwa, mpaka wakakutwa wamelala wakiwa kazini.

40 Nami nahofu ya kwamba itakuwa vivyo hivyo katika Kuja kwa Bwana. Kanisa limechukuliwa sana na kulewa na shughuli za ulimwengu, mpaka watakuwa wamelala kwenye wajibu wao, katika Kuja kwa Bwana.

41 Ndipo ndege zikaruka juu ya jiji, na mabomu yakaangushwa, nayo yakauponda-ponda tu mji huo, kabisa. Kwa nini? Kwa sababu hawangeweza kuzingatia onyo. Naye yule msichana, pamoja na hao wengine, wakati wale Wajapani, askari katili walipokimbia kuingia mle, waliwabaka mtaani, na kuwakata vipande-vipande kwa visu, baadaye, na kadhalika. Kwa maana kama hutazingatia onyo, limesalia jambo moja tu, hilo ni hukumu.

42 Loo, kama kuliwahi kuwa na wakati ambapo Marekani hii iliwahi kujidhalilisha kabisa, ni sasa hivi, juu ya utovu wake wa uadilifu, ya kutokujali kwake! Injili imehubiriwa kutoka pwani hadi pwani. Na ishara na maajabu yamefanyika. Na miujiza mikuu imefanywa, nao wanaendelea na shamrashamra zao, wakinywa pombe, wakipuza, wakifanya mizaha.

43 Kutoka kwenye mimbara laki mbili Marekani, za makanisa ya Kiprotestanti, tunachohitaji leo hii katika mimbara hiyo ni manabii wa Bwana, ambao hawaogopi kulipua radi za hukumu za Mungu juu ya kizazi hiki cha watu wenye dhambi

tunachohubiria. Tunahitaji manabii kama Isaya waliopaza sauti na kusema, “Kizazi kiovu!” Na jinsi ambavyo alikihukumu kizazi hicho, na kuwaambia juu ya hukumu zijazo.

⁴⁴ Lakini, siku hizi, wahudumu wetu wengi kupita kiasi wanaogopa kusema mambo hayo. Wanaogopa kutoa ushahidi wa moja kwa moja wa onyo, kwa maana ingemaanisha baadhi ya kazi zao. Wangelazimika kuacha madhehebu yao, kuacha mimbara yao. Na wangelazimika ku—kutoka nje, pengine, labda, na kuchukua msimamo mwingine kwenye kanisa lingine ama chochote kile. Lakini ni vibaya sana kwamba tuna watu wa aina hiyo kwenye mimbara zetu.

⁴⁵ Tunahitaji watu kama John Wesley, wa matengenezo ya awali, Martin Luther. Tunahitaji watu kama Paulo, ambao wako tayari kutoa yote, na kujisalimisha wenyewe, hata kama itamaanisha kutengwa na maisha haya, kama shahidi wa Injili ya kweli ya Yesu Kristo.

⁴⁶ Jambo ni kwamba, siku hizi, elimu na vyama na maskini mambo nyeti ya jamii, ya kuhangaisha, na hisia zao wenyewe, zimechukua mahali pa Roho Mtakatifu kanisani.

⁴⁷ Tunachohitaji, leo hii, kuililia Marekani, ni watu waliotumwa na Mungu, waliojazwa na Mungu kwa Nguvu ya Roho Mtakatifu, ambao hawaogopi kupiga makelele dhidi ya jambo baya, na kuwaonya watu juu ya hukumu ijayo.

⁴⁸ Mungu hangeweza kamwe kuruhusu taifa hili liepuke hukumu. Kama Mungu angefanya hivyo, ingemlazimu kuifufua Sodoma na Gomora, na kuwaomba msamaha kwa kuwazamisha, walipokuwa watu waovu hivyo. Sisi si—si tofauti mbele za Mungu. Mahali tumefikia leo hii, inapofikia siasa zetu, inapofikia serikali yetu, imeoza, kotekote. Hakuna haki tena, ila kwa Mungu tu.

⁴⁹ Loo, tunasema tunategemea U.N., Umoja wa Mataifa. Na zaidi ya miaka mitano iliyopita, walikuwa asilimia hamsini na moja wakomunisti, ya mataifa katika U.N. Hakuna cha kutegemea ila Neno la Mungu aliye hai. Hatuwezi kutegemea chochote sasa, hakuna siasa.

⁵⁰ Nimekuwa na kesi kwa miezi mitatu au minne iliyopita, chini ya moto mkali, wakijaribu kunishtaki kwa kufanya jambo lisilofaa, kwa kupitisha pesa katika maskani hii hapa, kwa ajili ya mikutano. Ambazo, halmashauri yetu ya wadhamini hapa ilitia sahihi azimio hilo. Wala hakuna mtu aliyewahi kuhudhuria mikutano yangu ila ambapo nimetangaza hadharani kwamba pesa hizi zilichukuliwa kwenye ninii yetu. . .katika mikutano yangu, zilipitishwa kwenye kanisa hili. Na sasa wanasema, ati kwa sababu nilizipitisha kanisani, nilikuwa nikijaribu kuibia serikali, na wanataka kunipa kifungo cha miaka ishirini huko Fort Leavenworth, Kansas, kwa ajili yake.

51 Nikasema, “Ni neno gani hilo lililoandikwa juu ya majumba yetu—yetu ya mahakama, ati ‘Haki’? Haina maana yoyote hata isingefaa kuandikwa hapo.” Kasema, “Huku kila kitu ambacho watu wenu waliniambia nifanye, nimefanya. Na sasa mnasema kwamba hawako pamoja na serikali tena. Mnawezaje? Mtatatua moja na kulithibitisha, halafu hapa watafukua kitu kingine.” Si hivyo tu, bali hawana msimamo.

52 Nilitoa tamshi hili katika mahakama za shirikisho. Nikasema, “Kama ukomunisti ungekuwa na Ukristo ndani yake, ningekuwa mkomunisti.” Lakini siwezi kuwa hivyo, kwa sababu unakana Ukristo.

53 Kwa hiyo nina mkono mmoja wa kushikilia, huo ni mkono wa Mungu usiobadilika, nikijua kwamba Yeye ataheshimu ukweli na heshima. Itabidi itokee, katika haki.

54 Lakini kukufanya ujue hakuna matumaini popote, ila katika Kuja kwa Bwana.

55 Loo, ni siku ya jinsi gani tunayoishi, wa—wakati mbaya sana! Wakati, kila kitu cha kimwili, hata kwa kanisa lenyewe, watu wa kanisa, madhehebu ya kanisa, wanazingatia sana tofauti za—zao ndogondogo, hata hawatashirikiana mmoja na mwingine, wala hawachukui onyo kwamba Kuja kwa Bwana kumekaribia.

56 Watu kama vile Billy Graham, na Jack Shuler, na Oral Roberts, na wengi wa wainjilisti wakuu, na Charles Fuller, walio na huduma ya ulimwenguni kote, wanafanya kila wawezalo, kutahadharisha juu ya Kuja kwa Bwana. Na hao watu wenyewe, hao watu wanaojaribu kufanya yaliyo mema, ndio watu ambao serikali yetu yenyewe inajaribu kuwararua vipande-vipande.

57 Nilimwambia mtu fulani, “Bwana, miaka ishirini na minane ya maisha yangu, nimelala kwenye madhabahu ya Mungu, kujaribu kufanya yaliyo mema. Nami ninataka mtu aniangalie kwenye jicho, aniambie ikiwa niliwahi kumtapeli mtu yeyote chochote, au niliwahi kuiba chochote maishani mwangu. Kwa neema ya Mungu, sina hatia.”

58 Hilo halimaanishi zaidi, kwake, zaidi ya kudata kidole chako. “Una hatia, hata hivyo! Nawe ni dikteta katika kanisa lako! Unadata kidole chako nalo kanisa lako linafanya kile unachowaambia wafanye!”

“Loo,” nikasema, “watu wanaweza kuwa dhalimu jinsi gani?”

59 Akasema, “Uliwapa watu zawadi wakati nyumba zao ziliteketea. Hizi hapa hundi zako ambapo uliwapa wajane mamia ya dola, na kuwalipia kodi ya nyumba, na kufanya mambo kama hayo.” Kasema, “Je, ulienda kwa halmashauri yako ya kanisa na kuwaambia utafanya hivyo?”

Nikasema, “La, bwana.”

“Kwa nini hukuwaambia?”

⁶⁰ Nikasema, “Bwana aliniambia, katika Neno Lake, ‘Usiruhusu wa kuume . . . mkono wako wa kushoto ujue ufanyalo mkono wako wa kulia.’”

⁶¹ Akasema, “Basi unajaribu kuitetea kesi yako kwa Biblia, nasi tunakuhukumu kwa sheria.”

⁶² Nikasema, “Sheria ya juu zaidi ni ipi, ya mwanadamu au ya Mungu?” Nitachukua sheria ya Mungu.

⁶³ Miaka michache tu, miwili iliyopita, nilikuwa kwenye likizo yangu, nilikuwa njiani nikirudi.

⁶⁴ Hapa Indiana kanuni za spidi ni maili sitini na tano kwa saa wakati wa mchana, na hiyo ni kwenye barabara kuu huru, barabara huru. Na ni maili sitini kwa saa wakati wa usiku, jua likiisha kutua. Ndivyo ilivyo huko Kansas. Ndivyo ilivyo Illinois. Ndivyo ilivyo Colorado. Ndivyo ilivyo Idaho. Ndivyo ilivyo Wyoming.

⁶⁵ Basi wakati nikirudi, baada ya kukaa kwenye chungu cha theluji kwa siku kadhaa katika dhoruba kali ya theluji; nami nilikuwa nimempata kulungu hivi punde tu, nami nilikuwa nikienda nyumbani, kuwapa marafiki zangu. Basi ilinibidi kuharakisha kujaribu kukwepa kimbunga kingine kilichokuwa nyuma yangu tu, la sivyo ningezuiliwa tena, nayo hiyo nyama ingeharibika.

⁶⁶ Nami nilikuwa nimevuka Wyoming, nikaingia Nebraska. Nilikuwa yapata maili thelathini juu, ndani, barabarani. Na kwa ghafla, nikatazama nyuma, nikaona kimulimuli chekundu cha polisi. Na sikuwahi kukamatwa maishani mwangu. Kwa hiyo, niliendelea tu. Nikaangalia chini, nilikuwa ninaenda maili sitini kwa saa, nje kwenye ma . . . maili thelathini au arobaini kutoka kwenye m—mji wa aina yoyote. Nikishuka tu kwenye barabara kuu, barabara kuu ya njia nne. Ndipo, nikaona, maili sitini kwa saa. Nikatazama nyuma, naye akaendelea kubaki nyuma yangu. Nami nikaangalia tu.

⁶⁷ Ndipo nikaona kimulimuli chekundu kikimulika, nikawazia, “Vema, kwa nini asinipite? Ana nafasi kubwa.” Nami nikaendelea kusubiri. Nikateremsha dirisha langu chini, ndipo nikasikia king’ora. Vema, nikawazia, “Niko kando kadri niwezavyo kuwa.” Ndipo akaja karibu na kunisimamisha.

⁶⁸ Nikatoka kwenye gari. Nikawazia, “Labda kuna ujumbe ambao sikuupokea kwenye redio, labda nyumbani, mke wangu au familia.” Nami nikashuka kwenye gari hilo, bila fununu niwezavyo kuwa.

Akasema, “Nadhani unashangaa ni kwa nini nimekusimamisha?”

Nikasema, “Naam, bwana.”

⁶⁹ Naye akasema, “Ulikuwa unavunja kanuni za spidi.” Kasema, “Unajua ulikuwa ukienda mbio kiasi gani?”

Nikasema, “Naam, bwana.” Nikasema, “Nilikuwa nikienda maili sitini kwa saa.”

Akasema, “Hiyo ni kweli. Na hiyo ni kinyume na sheria.”

Nikasema, “Kwani si ni sitini na tano katika . . . ?”

⁷⁰ “Hapana, bwana.” Kasema, “Ni hamsini na tano hapa. Ulikuwa ukiendesha maili tano juu ya kikomo rasmi cha spidi.”

“Loo,” nikasema, “Samahani. Sikulimaanisha.”

⁷¹ Kasema, “Nipe leseni yako ya udereva. Nionyeshe tu leseni yako.”

⁷² Basi nikazitoa mfukoni mwangu. Na mara tu alipoona neno hilo ‘kasisi,’ macho yake yaliwaka moto. Akanyakua kitabu chake na kuanza kuniandikia tiketi ya dola ishirini na nne na senti hamsini.

Nikasema, “Utanipa tiketi?”

Kasema, “Umesema kweli! Nitakupa tiketi!”

“Vema,” nikasema, “bwana, ni sawa. Lakini sikuona chochote.”

⁷³ Akasema, “Loo, kuna ubao papo hapo mpakani mwa mkoa. Ulipaswa uwe umeuona.”

⁷⁴ “Vema,” nikasema, “nimekuwa nikiketi kwenye ninii nne . . . chungu cha theluji siku nne, na inawezekana sikuuona, bwana.”

Naye akasema, “Vema. Je, una pesa taslimu?”

Nikasema, “Takriban dola kumi na mbili.”

⁷⁵ “Vema,” akasema, “utakaa papa hapa mpaka utakapolipa.” Yapata saa nne usiku, au tano.

⁷⁶ Nikasema, “Bwana . . .” Nikamwambia yote, shida yake, na nyama na kadhalika. Hilo halikumaanisha kitu kwake. Kwa hivyo ilinibidi kusaini taarifa ya uaminifu, kwamba nitawatumia hizo pesa.

⁷⁷ Nilipofika nyumbani, nilimwandikia hakimu, wa huo mji mdogo, maskini hakimu yule niliye paswa kumtumia. Nami nikamwambia. Nikasema, “Bwana, nimetumia ninii ishirini na . . . kama miaka ishirini na mitano,” wakati huo, “miaka ishirini na sita katika utumishi wa Bwana, nikijaribu kuwabadilisha wahalifu kwa Bwana Yesu, kujaribu kuyalinda maisha yako kama ofisa, kujaribu kuunda jamii bora, na mahali bora pa kuishi, na adabu kwa familia zetu. Nimetumia miaka ishirini na kitu katika huduma hiyo. Nami nilivuka tu mpaka wako. Naona kwamba unapaswa kunisamehe hilo.” Nikasema, “Lakini ofisa wako hata hangenifikiria, hata kidogo. Ambapo, labda anapaswa kufanya hivyo, na kutekeleza wajibu wake. Lakini nakuomba, kama hakimu. Sio pesa; ni kanuni. Faini

yangu ya kwanza niliyopata kulipa, na hizi hazina budi kutoka kwenye pesa ambazo watu wananipa kama riziki, kupitia kwa kanisa.” Nikasema, “Iwapo utakuwa mwema kiasi cha kunisamehe hilo, nitashukuru. Hata hivyo, hii hapa hundi ambayo imethibitishwa, upate kujua kuwa ni—ni nzuri.”

⁷⁸ Ndugu, alisaini tu jina lake juu yake na kuipokea, kikatili. Kwa nini? Kwa nini? Na halafu, kupitia siasa mbovu, na ubaguzi wa kidini, baadhi yao hukwepa na mauaji. Hilo hapo.

⁷⁹ Mungu hataruhusu Kanisa Lake kuwepo kwa muda mrefu chini ya mambo kama hayo. Nayo dunia imeoza. Na siasa imeoza. Na kanisa limeoza. Tunachohitaji, kufanya mengi kwake, ni watu wanaomcha Mungu kukusanyika pamoja na kuliitia Jina la Bwana. Hivyo ndivyo Maskani ya Branham inahitaji kufanya. Loo, napenda . . .

Kuangalia tu na kuona nilikuwa na mengi mbele yangu.

⁸⁰ Na kutafakari ni kiasi gani tunachoweza kusisitiza hapa, jinsi kanisa linavyoendelea; jinsi walivyodhalilisha maadili ya watu, jinsi wanavyowaacha waishi, na kwenda kwenye madansi na roki, na kuvaa vyovyote wapendavyo, na—na kila kitu, na bado wanaendelea vivyo hivyo, wahubiri wenye kupatana.

⁸¹ Tunachohitaji ni wahubiri wa mtindo wa kale, waliotumwa na Mungu, waliozaliwa kutoka Mbinguni ambao watasema Kweli bila kujali inaumumiza nani. Kama Yohana, ambaye alisema, “Shoka limewekwa kwenye shina la mti.” “Na kila mti usiozaa matunda mazuri unakatwa na kutupwa motoni.” Tunahitaji wahubiri, manabii kama hao, ambao watashambulia, na kutumia hukumu za Mungu kama makombora, kurarua, katika hali hii ya kuchukiza tunayoishi.

⁸² Huwezi kamwe kuiondoa dhambi kwa kuipapasa mgongoni. Kamwe huwezi kuondoa dhambi kwa kuwaelimisha watu. Mipango yetu imebomolewa na imeshindwa. Kuna tiba moja tu kwa ajili ya dhambi, na, hiyo ni, Kristo ndiye tiba hiyo. Wala sio Kristo kupitia maungamo ya kiakili, bali kupitia ubatizo wa Roho Mtakatifu, hadi kwenye Maisha mapya na kuzaliwa upya. Hiyo ndiyo tiba pekee ya dhambi, tiba pekee kwa taifa. Ndiyo tiba pekee kwa kanisa. Ndiyo tiba pekee kwa watu.

⁸³ Hapa siku moja . . . Nadhani wengi wenu ninyi mnaosafiri mmekuwa huko. Nimekaa huko usiku kucha mara nyingi, katika safari yangu ya kwenda Magharibi. Ambako inanibidi niende juma lijalo, faraja, nipate shime ya kwenda kutoka kwa serikali. Wananiishikilia hapa. Ambapo, kama wangeniachilia niende, wangeweza kunipata papa hapa. Nami sina budi kwenda kwenye mikutano kadhaa huko kwenye Pwani ya Magharibi. Na Bwana akipenda, nitapitia kwenye mji huu mdogo uitwao Memphis Magharibi, Arkansas. Ni ng’ambo tu ya mto kutoka Memphis, Tennessee. Basi mahali hapa walitaka kutumia dola milioni mbili na nusu kwa uwanja wa mbio, kuchezea kamari.

Dola milioni mbili na nusu, ili kuwadhalilisha, na kuwachafua, na kuwapeleka watu kuzimu. Na kisha wawakamate watu kama Billy Graham, Oral Roberts, mimi mwenyewe, na wale wanaoteseke kwa ajili ya Kristo, kupitisha pesa halali kanisani, na kutaka kuwafunga miaka ishirini katika gereza la shirikisho. Daima imekuwa ni mapenzi ya ulimwengu kutenda hivyo.

⁸⁴ Nikasema, “Wewe. . . Ninao ndugu ambao wamekuwa katika gereza la shirikisho.”

⁸⁵ Ndipo mmoja wa mawakili hao akasema, “Ati una ndugu katika gereza la shirikisho?”

Nikasema, “Nilikuwa nao.”

Kasema, “Walikuwa akina nani?”

⁸⁶ Nikasema, “Mmoja wao alikuwa Ndugu Yohana, huko Alkatrazi, kwenye kisiwa cha Patimo. Na huyo mwingine alikuwa Ndugu Paulo, katika gereza la shirikisho la Kirumi. Na Ndugu Danieli, yeye pia alikuwa katika nyumba ya gereza.”

⁸⁷ Na Ndugu Yusufu, kwa sababu alikuwa ameshtakiwa jambo ambalo hakuwa na hatia, alitumikia kifungo kwa miaka mingi, kwa kujaribu kuwa mtumishi halisi wa Potifa, ndipo mkewe akamshtaki. Naye akahukumiwa, na kuwekwa gerezani kwa miaka mingi, mpaka masharubu yake na nywele zake zikamea, hata hakuninii. . . Hata iliwabidi kumnyoa, wapate kumpeleka mbele ya Farao. Hakika. Kwa nini, kitu chochote kibaya? Kwa ajili ya Kristo! Hasa!

⁸⁸ Halafu watumie dola milioni mbili na nusu kwa uwanja wa mbio, kuchafua na kulaani na kuwapeleka watu kuzimu. Wakizungumza juu ya Mungu kuja haraka!

⁸⁹ Lakini watu wa Arkansas walifanya jambo fulani kuhusu hilo. Kila kanisa, nafikiri, madhehebu tisa ama kumi mbalimbali katika jumuiya hiyo, wote wakakusanyika pamoja na kusema, “Ni makosa. Wala hatukitaki.” Ndipo wakafanyiza mkutano wa maombi, nao wanachukua mifululizo ya maombi, mchana kutwa, na usiku kucha. Ndipo wakati mahakimu na watu wa shirikisho, basi wote walipoenda mahakamani kesho yake asubuhi, kulitatu, iwapo wangeweza kuujenga au la, walikutana, na ikashindwa. Maombi hubadilisha mambo. Sijali jinsi ulimwengu ulivyooza, jinsi nchi yetu ilivyooza, taifa letu, watu wetu; maombi yetu hubadilisha mambo.

⁹⁰ Lakini hatuvutiwi na mkutano wa maombi tena. Tuna mambo mengine mengi tunayopaswa kufanya, ndivyo tunavyowazia.

⁹¹ Halafu basi, isitoshe, uwanja huo wa mbio haukukumiwa tu, bali pia iliamriwa kwamba, katika wilaya ya Arkansas, wasingeweza kuwa na kitu kama hicho tena kwa miaka na miaka ijayo. Kwa nini? Kwa sababu watu wanaoitwa kwa Jina Lake hukusanyika pamoja na kuomba.

⁹² Loo, tunachohitaji leo ni kuitwa pamoja, kujitayarisha. Wala si kumtegemea mhubiri, bali wewe, kama mtu binafsi mbele za Mungu, kujiweka tayari kwa ajili ya Kuja kwa Bwana, kuepukana na uharibifu huu wote.

⁹³ Haijalishi wanakuitaje, na wanachukua hatua gani, hiyo haimbadilishi Mungu hata kidogo. Mungu atalifanya, vivyo hivyo tu. Anatutegemea na kutungojea sisi. Loo, jamani!

⁹⁴ Baadhi ya watu wanasema, “Vema, mimi huenda kanisani Jumapili asubuhi. Ninamsikiliza mchungaji wetu, ambaye ni mhubiri mzuri.” Hilo ni jema. Nathamini hilo. Na wewe ndiwe Marekani, ulimwengu, yeyote yule. Lakini inahitaji zaidi ya ujumbe mzuri kutoka mimbarani. Inahitaji maisha yako. Inakuhitaji wewe, kuwa tayari.

⁹⁵ Katika Ufunuo mlango wa 19, na kifungu cha 7, Biblia ilisema ya kwamba, ikinena juu ya Bibi-arusi wa Kristo, “Amejiweka tayari.” Alijiweka tayari Mwenyewe. Nawe, kama mshiriki wa Bibi-arusi huyu, huna budi kujiweka tayari.

⁹⁶ Wakati fulani uliopita, mhudumu mmoja alikuwa akihubiri. Na—na kulikuwa na mtu ambaye alikuwa akihudhuria kanisa lake kwa, loo, kwa muda mrefu sana. Basi alikuja asubuhi hiyo mpaka madhabahuni. Naye akasema, “Mchungaji, sasa nataka kutoa ushuhuda wangu na kujitolea kwangu kwa Bwana Yesu, jambo ambalo nimefanya jana usiku.”

⁹⁷ Naye mchungaji akasema, “Vema, hakika nimefurahi kusikia kuhusu hilo, John. Kujua kwamba umeamua hatimaye kuja na kujitolea kwa Bwana, kwa sababu hatutaki kuumiza hisia zako, lakini tunajua kwamba umekuwa mwovu sana. Pia tunajua umeitesa familia yako. Umechezea pesa zako kamari, na ukazinywea pombe, na kuishi maisha ya kutisha, na familia yako ikakaa bila. Basi linaupa moyo wangu furaha, asubuhi ya leo, kujua kwamba umejitokeza sasa na utajisalimisha kwa Bwana Yesu, kuwa mtu tofauti, kumtumikia Yeye.”

Akasema, “Asante, mchungaji.”

⁹⁸ Akasema, “Basi ni nini. . . Nataka kukuuliza jambo fulani. Nilihubiri mahubiri gani, au nilitumia andiko gani, na, au ni wimbo gani ulioimbwa kanisani, katika tenzi, ambao ulikufanya uamue kufanya hivi?”

⁹⁹ Basi wakati yule mtu akimtazama usoni, huku machozi yakitiririka mashavuni mwake, alisema, “Mchungaji, hayakuwa yoyote ya mahubiri yako, hata hivyo, kadiri yalivyokuwa mazuri. Haikuwa moja ya kwaya ikiimba, au nyimbo maalum, ingawa zilikuwa ni nzuri.”

¹⁰⁰ Akasema, “Basi unaweza kuliambia kusanyiko hili kwa nini umefanya uamuzi huu?”

¹⁰¹ Akasema, “Ninafanya kazi na mtu ambaye ni Mkristo, na nimemwambia kila kitu. Nilimwita mtakatifu anayejibingirisha.

Nilimwita shupavu wa dini na kila kitu, wala halikumsumbua hata kidogo. Lakini aliishi maisha mazuri sana hata hatimaye, moyoni mwangu, wakati wote, amepata mahali fulani, hata ninataka kuwa kama mtu huyo. Na hiyo ndiyo sababu nilimwomba aniongoze kwa Kristo. Nilimtaka yule Kristo ambaye yeye anamtumikia.”

¹⁰² Mnaona, Mungu kweli hufanya kazi kupitia kwa mchungaji, kulifanya tayari Kanisa Lake. Anafanya kazi kupitia nyimbo, kulitayarisha Kanisa Lake. Pia anafanya kazi kupitia kwako, kulitayarisha Kanisa Lake.

¹⁰³ Kama mchungaji wako angeshindwa, na aendeleo kushindwa, ungejitafutia mchungaji mwingine. Upesi ungefanya hivyo. Endapo kwaya yenu haikuimba vizuri, au uimbaji wenu wa mtu mmoja mmoja haukuwa sawa, ungemwambia mwongozaji, yule aliye na muziki, “Usiwaruhusu kuimba tena. Wananifanya tu nichanganyikiwe, wakiimba.”

¹⁰⁴ Lakini vipi wewe kama mtu binafsi? Unashindwaje katika maisha yako ya kila siku? Je, unajifaninishaje na Mungu, kile Mungu anachosema uwe, Nuru ing’aa iliyouwekwa kilimani? Hakuna mtu anayeweza kupita njia hiyo, vema, karibu na njia yako, pasipo kujua habari za Yesu. Je, unaishi maisha ya aina gani, mojawapo ya aina hizo ambayo ni mabaya, ya matusi, na ya kuudhi, kutojali? Au, unaweza kuzungumza juu ya amani na upendo ambao umeupata katika Kristo?

“Amejiweka tayari.”

¹⁰⁵ Nimewaonyesha ukatili. Wala wakati haungeweza... ungenipungukia, kupitia nyakati, na kuonyesha kwamba kila wakati, kama vile kule Babeli katika ule usiku wa zile shamrashamra, na kucheza dansi na kunywa pombe, na kadhalika, na yale yaliyotukia. Na kote katika wakati imekuwa hivyo. Katika kila wakati Mungu amekuwa na manabii jasiri wasiozuilika, pamoja na ishara na maajabu, kulaani jambo hilo katikati ya umaarufu wote, na kusimama peke yao kwa ajili ya Mungu.

¹⁰⁶ Isitoshe, lakini vipi kama ngingezungumza kuhusu wakati wa maskini Stefano, sio nabii, sio mchungaji, mshiriki tu wa Mwili wa Kristo. Jinsi maskini jamaa huyu mdogo alivyosimama mbele ya Baraza la Wazee asubuhi ile, akanena dhidi ya wale waliokuwa wakimhukumu, na kusema, “Enyi wenye shingo ngumu, msiotahiriwa moyo wala masikio. Sikuzote mnampinga Roho Mtakatifu. Kama baba zenu walivyofanya, nanyi ni vivyo hivyo.” Hakuwa mchungaji.

¹⁰⁷ Huwezi kumtarajia mchungaji wako afanye yote. Huwezi kutarajia halmashauri yako ya wadhamini kufanya yote, wala halmashauri yako ya mashemasi. Inabidi ujiweke tayari. Ni jambo la mtu binafsi.

¹⁰⁸ Pia, kumbukeni, Kuja Kwake ni kwa ghafula sana, hata Kanisa litaondoka katika kufumba na kufumbua jicho. Na kama tunaona dhambi kila mahali, na hukumu ikingojea, na manowari za ghadhabu ya Mungu zikija, je, tutapataje kuikwepa hii? Ishara zinaonekana. Yesu yuaja. Na maajabu makubwa yanafanyika. Kila nguzo ya maili inaelekeza kwenye kuonekana Kwake hivi karibuni, na kutatokea katika dakika moja.

¹⁰⁹ Je, tumesimamaje, asubuhi ya leo, tunapofanya hesabu? Kama tungezungumziwa, asubuhi ya leo, na Bwana Yesu akashuka kutoka mbinguni, asubuhi ya leo, na Mwaliko pamoja na Parapanda ya Mungu, je, tungepatikana tayari, kama kundi la kanisa? Je, tungepatikana tayari, kama mtu binafsi, kuungana na wale waliofufuliwa kutoka kwa wafu, ambao wamejidhihirisha kuwa tayari? Haijalishi kama tuko tayari au la, Bwana Yesu atakuja vivyo hivyo tu, kwa wakati uliowekwa. Hatuna budi kuwa tayari, na lazima tufanye hivyo sasa. Sio wakati wa kusubiri. Ni lazima tuokoe wakati na kuwa tayari.

¹¹⁰ Siku moja, hadithi (kabla tu ya kufunga) ambayo ilinigusa, nilipoisikia, miaka mingi, mingi sana iliyopita.

¹¹¹ Kuja huku kwa siri kwa Bwana; kuondoka ghafla, kwa siri kwa Kanisa. Tazameni! “Wawili watakuwa kondeni; nitamtwaa mmoja na kumwacha mmoja. Wawili watakuwa kitandani; nitamtwaa mmoja na kumwacha mmoja.” Ikionyesha ya kwamba Kuja kwa Bwana hakutakuwa tu kwenye kona fulani, bali kutakuwa kwa ulimwengu wote. “Mmoja atakuwa kondeni, akifanya kazi,” mchana. “Huyo mwingine atakuwa kitandani, amelala,” upande wa pili wa dunia. Utakuwa Unyakuo wa ulimwengu mzima, nao utakuja na Mwaliko, pamoja na Sauti ya Malaika Mkuu, na Parapanda ya Mungu Italia. Na waliokufa katika Kristo watafufuka. Naye atanyakuliwa, kwa siri. Loo, ninapenda hilo! Bwana-arusi mkuu anakuja, na Bibi-arusi amejiweka tayari, akingojea wakati huo wa siri ambao hata haujui, Mwenyewe. Lakini yuko tayari, na amejivika mavazi, huku akingojea.

¹¹² Tunaona vibao Vyake vya matangazo ulimwenguni, ya kwamba yuko tayari kwa hukumu. Tunaona ishara na maajabu kanisani, mambo makuu yakitukia. Je, tunapaswa kuwa watu wa aina gani? Tayari kwa wakati huu, kwa maana hatujui atakuja lini. “Nanyi pia jiwekeni tayari, kwa maana hamjui saa ambayo Bwana wenu atakuja.” Iweni tayari! Kwa kuwa, huwezi kujiweka tayari wakati huo, kwa maana Yeye alisema usingeweza.

¹¹³ Ni wangapi kati yenu, labda wote, wamesoma juu ya wale wanawali? Wengine walikuwa wenye busara na wengine wapumbavu. *Mwanamwali* anamaanisha “usafi.” Wote walikuwa watu wema. Kila mmoja wao, mwanamwali, vyombo vilivyotakaswa vya Mungu. Lakini wale waliokuwa na Mafuta

katika taa zao, waliingia, na hao wengine wakaachwa nje. Wote walikuwa wanawali, kila mmoja. Watu ambao usingeweza kuwaelekezea kidole chako, kwa chochote kibaya. Wao, kila mmoja, waliamini katika Kuja kwa Bwana. Walikuwa tayari kwenda kumlaki, lakini baadhi yao waliacha Mafuta yao yaishe.

¹¹⁴ Usiruhusu hiyo iwe ndiyo hali yako. Tia Mafuta katika taa yako. Mafuta ni Roho, Roho Mtakatifu. Usiache ikuishie. Unapohisi upendo wako ukifa, uaminifu wako kwa Kristo na kwa—kwa Huduma, upesi nenda Kwake Yeye aliye na chemchemi ya Mafuta, na ujinunulie ujazo wa Roho Mtakatifu.

¹¹⁵ Taifa letu limekwisha, limepotoka kimaadili na kuharibika. Siasa zetu, zimeharibika na zimekwisha. Viongozi wetu, Ee Mungu, tungefanya nini kuhusu hilo? Unaweza kumwingiza mtu mzuri, na anatoka laghai.

¹¹⁶ Kuna Mmoja tu tunayeweza kumleta sasa, huyo ni Bwana Yesu. Hebu tujitayarishe kwa ajili ya Kuja Kwake.

¹¹⁷ Ninataka kuwasimulia hadithi ndogo ambayo nilisikia miaka kadhaa iliyopita; tukifunga. Unyakuo huu wa ghafla, wa haraka wa Kanisa!

¹¹⁸ Sasa unasema, “Mambo fulani yatatukia, ndipo nitajiweka tayari.” Jiweke tayari sasa. Nimewasimulia hivi punde kuhusu Bandari ya Pearl na sehemu nyingi ambapo walikataa kusikia onyo. Walikataa kulisikiliza. Hakuna kilichosalia ila hukumu ya Kiungu juu ya watu. Sasa, wote ambao hawataingia katika Kristo watakuwa chini ya ghadhabu ya Mungu na hukumu ya Kiungu. Tafadhali usiruhusu hilo likupate.

¹¹⁹ Haidhuru Maskani ya Branham itaishia kuwa nini, usiruhusu iwe ni wewe. Wewe kuwa mtumishi wa Kristo. Haijalishi ulimwengu wa kanisa unafanya nini, wewe kuwa mtumishi wa Kristo. Si juu ya Maskani ya Branham, wala si juu ya kanisa lingine lolote. Ni juu yako, kama mtu binafsi, kuwa tayari kwenye Kuja kwa Bwana. Lazima uwe tayari. Lazima niwe tayari. Nitafagia vipandio vyangu mwenyewe. Ni juu yako kufagia vipandio vyako. Achana na vyangu; nami niachane na vyako. Huna budi kuweka tayari vazi lako.

¹²⁰ Kulikuwa na mwanaranchi mkubwa, naye alikuwa na ranchi kubwa mno, huko mbali sana katika sehemu ya kaskazini mwa Colorado, karibu na ile sehemu ya mlima.

¹²¹ Kama nyote mjuavyo, nimefanya ufugaji kidogo maishani mwangu, wa kuwafunza farasi na kadhalika. Moja ya wito wangu kwa Mungu, ulikuwa ni kuketi juu ya jozi ya vichokoo vya kale vya magurudumu ya Teksas, huku bunduki imewekwa juu ya tandiko na bastola ubavuni mwangu; niliposikia hiyo miti ikivuma, ilisikika kama Sauti iliyosema, “Adamu, uko wapi?”

¹²² Ndipo nilipoangalia juu kwenye nyota, nikamsikia mzee Slim, kaoboi mzee kutoka huko Teksas, akipulizia kichanuo

kwa kipande cha karatasi (Huko chini msalabani alikofia Mwokozi wangu, huko chini ndiko nilikolilia nitakaswe kutoka dhambini; Pale moyoni mwangu Damu Yake ilipakwa; Utukufu kwa Jina Lake), niliufunika uso wangu kwa blanketi na kujaribu kujificha, kwa maana Mungu alikuwa akitazama chini katika vilima hivyo.

¹²³ Ilikuwa kwenye moja ya ranchi hizo, ambapo kampuni kubwa za upakiaji hununua ng'ombe wao, wanawapeleka milimani, na kisha wanawashusha ndama chini wakiisha kuzaliwa, kwenye—kwenye msimu wa majani kupukutika, na kuwapiga chapa, na kuuza baadhi ya ng'ombe wakubwa, na maksai na kadhalika, na kuendelea mbele katika...kupanua makundi yao makubwa ya ng'ombe.

¹²⁴ Na kwenye ranchi hii fulani, mmiliki, au mtunzaji, tunayemwita kule, “mkubwa,” msimamizi, alikuwa na yapata mabinti watano. Wote walikuwa wanawake warembo, vijana, hawajaolewa.

¹²⁵ Basi kulikuwako na msichana mdogo kule, ambaye alikuwa binamu wa wasichana hawa, ambaye baba na mama yake pia walikuwa wamefariki. Naye aliletwa kule kuwa...kuishi na a—amu yake.

¹²⁶ Na hao wasichana, ambao walivikwa aina hizo za gauni zilizorembeshwa kwa mapambo, mwajua, na—na—nao wakamchukua tu maskini msichana huyu mdogo kumtendea tu kana kwamba alikuwa ni mnyama fulani. Kazi ngumu yote alimwagiliwa yeye. Aliosha vyombo. Alifanya usafi. Akatengeneza vitanda. I—ilimbidi afanye yote. Nao waliketi tu kitako na makucha yaliyong'arishwa na kupakwa rangi, vile vitu midomoni mwao, na wamejinadhifisha vilivyo, warembo kweli.

¹²⁷ Na hasa walifanya hivyo waliposikia kwamba kutoka Chicago, ile kampuni kubwa ya upakiaji iliyomiliki mahali hapo, mwanawe mdogo, mseja alikuwa anakuja kuitembelea hiyo ranchi. Loo, kweli walijitokeza katika mavazi mazuri! Aha! Na kweli walijivika na kujiweka tayari kwa ajili ya kuja kwake! Na kila usiku mazungumzo yangukuwa, walikuwa wanaenda kumfanyia ubembe kijana huyu wapate kuolewa naye. Ambao wangeninii...Ndipo wangeimiliki hiyo ranchi, wao wenyewe, kwa kuwa huyo mwana angeirithi yote. Kwa hiyo wakajiweka tayari.

¹²⁸ Kwa hiyo, mnaona, kuna maandalizi yanayohitajika. Ukijifanya tayari, kwa kujiunga na kanisa ama chochote kile, hayo si yote yanayohitajika. Huna budi kuwa na Mafuta katika taa yako. Unaona? Mavazi yako tu, kusema, “Tutajenga kanisa kubwa. Tutakuwa wafuasi wa dhehebu bora zaidi. Tuta—tutajinunulia kinanda kidogo, kwa ajili ya

Bwana. Tutatengeneza viti vya kifahari.” Hicho sicho Mungu anachohitaji.

¹²⁹ Haki ndiyo Mungu anayohitaji, katika Mwanawe, Kristo Yesu. Hayo ndiyo mavazi. Kwa maana Biblia ilisema, “Mavazi meupe ambayo amevikwa, ni haki ya watakatifu.” Hivyo yeye. . .

¹³⁰ Wasichana hawa walidhani watajiweka tayari kwa kuja kwa kijana mwanamume huyu. Bila shaka, maskini binamu huyo, hiyo inanikumbusha mtu aliyekataliwa mahali fulani. Ungeweza kumthamini. Alikuwa mwanamke mrembo. Lakini, loo, jamani! Alikuwa msichana mdogo mzuri, lakini hata hakuhesabiwa miongoni mwao, si kama jamaa.

¹³¹ Sasa hiyo ni kama picha halisi ya Kanisa halisi, siku hizi, mbele ya madhehebu. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Hata halihesabiwi; kundi la wasiojifunga na madhehebu, kundi la watu waliotengwa na jamii.

¹³² Kwa hiyo maskini jamaa huyo aliendelea tu, akifanya kazi. Ndipo yule kijana mwanamume alipowasili. . .

¹³³ Hawakujua, lakini alikuja kutafuta mke. Alikuwa amechoshwa kabisa na wasichana wa mjini ambao walikaa tu wamejipamba, na, loo, unajua, walirandaranda karibu na baa, na kuzunguka kwa kadilaki, na ma—mambo mbalimbali. Wa—walikuwa wamechoshwa tu kabisa nayo. Akawazia, “Nitaenda huko Magharibi na kujitafutia m—msichana halisi ambaye atakuwa mama halisi kwa watoto wangu. Na mtu ambaye hatarandaranda kwenye makundi yote ya kushona na—na vyama na kadhalika, lakini atakuwa mama halisi.” Alipata nini alipofika kule, ila kitu kile kile alichokuwa amekihukumu kule Chicago?

¹³⁴ Sijui kama Bwana Yesu atakuta kanisa, dhehebu tu, kwa jina tu, “kanisa,” lisilo na Mafuta katika taa, lisilo tayari kwenda? Loo, wana magauni mazuri. Wana makanisa makubwa zaidi, *ninii* kubwa zaidi, na mambo haya yote. Lakini Mungu hataki hilo. Anakutaka wewe kama mtu binafsi. Wanaweza wakawa na wachungaji bora zaidi, wanaweza wakawa na halmashauri bora zaidi ya mashemasi, lakini Yeye anakutaka ukiwa na Mafuta. Anakuja kuyanyakua hayo Mafuta na Bibi-arusi.

¹³⁵ Naye, mvulana huyu, alipowatazama, alivunjika moyo. Basi usiku huo walikuwa na kitu mfano wa. . . Katika siku hizo, imekuwa zamani sana, waliita “Charleston,” ambayo ni kama tu roki. Nao walikuwa wanaenda kufanya moja ya karamu hizo kubwa. Wengi wenu ninyi watu mnakumbuka ile dansi ya kale ya Charleston waliyocheza, huko nyuma nilipokuwa mtoto, nilipokuwa huko nje. Na kwa hiyo wote walikuwa wamevaa nguo zao ndogo nyeusi na nyeupe, mwajua, kufanya ninii. . . Loo, iliitwa “Charlestons,” na “kikalio cheusi.” Hivyo

ndivyo zilivyoitwa. Nao walikuwa na nguo za rangi mbili, nao wangefanya ngoma hizi.

¹³⁶ Na, lakini, mvulana huyu alikuwa amechoshwa na upuuzi huo. Alikuwa anamtafuta msichana halisi, hivyo akaiacha karamu yao kisiri. Alikuwa akiwatazama. Akaingia ndani kuwaangalia.

¹³⁷ Vivyo hivyo na Mwana mwingine ninayemjua. Mwana mwingine atakuja kanisani mwenu. Ataninii... Mwana wa Mungu, atakuja kule. Ataangalia pande zote. Atakuona umevaa vizuri. Ata—atajua kuwa wewe ni mshiriki mzuri. Lakini Yeye anatafuta kitu tofauti na mwenendo wa kawaida wa kanisa.

¹³⁸ Kwa hiyo alipotazama huku na huku, baada ya kitambo kidogo, alivunjika moyo sana. Akatoka mlangoni.

¹³⁹ Ndipo akirudi, akitembea katika mbalamwezi, kuelekea kwenye nyumba ya wafanyakazi, alisikia mtu fulani akivumisha wimbo. Naye akatazama pande zote. Naye huyu hapa maskini msichana mmoja na sufuria kubwa ya maji ya vyombo, usiku sana, bila viatu, kumwaga maji ya vyombo nje. Na mara tu alipomwona, kitu fulani kikasema, “Huyo ndiye. Huyo ndiye.” Kwa hiyo akajiweka njiani. Na wakati huyo msichana... Hapo ndipo aliporudi kupitia kwenye ua la hilo boma, mbona, yeye alikuwa amesimama pale. Naye nusura azimie.

¹⁴⁰ Akasema, “U hali gani?” Kisha akasema, “Jina lako nani?” Naye akamwambia jina lake, na lilikuwa ni jina lile lile la bosi wa ranchi hiyo. Kasema, “Basi siwezi kuelewa jinsi huyu... Je, huyo ni baba yako?”

¹⁴¹ Kasema, “La. Mimi ni binamu tu, unaona. Yeye na baba yangu walikuwa ni ndugu. Nina jina lile lile. Lakini mimi... Huyo, huyo ndiye bosi.”

¹⁴² Unaweza ukawa na jina la kanisa, unaweza ukawa na jina la Maskani ya Branham, ama Methodisti, ama kanisa lolote unalohudhuria. Hilo silo, rafiki. Unaona? Ni kitu tofauti. Ni tabia yako. Hiyo ndiyo Mungu anaangalia. Unaweza ukawa Mmethodisti. Unaweza ukawa Mbaptisti. Unaweza ukawa Mpresbiteri. Hilo silo. Tabia ndiyo Mungu anayoangalia. Si tu tabia ya kidunia, bali tabia ya Roho Mtakatifu. “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio,” alisema Yesu, katika mlango wa 16 wa Marko Mtakatifu.

¹⁴³ Alishangaa sana kwamba—kwamba hata angezungumza naye. Naye akakinamisha maskini kichwa chake chini, na kuingia nyumbani mbio.

¹⁴⁴ Alikuwa huko kwa juma moja au mawili, naye akaangalia pande zote, kila mahali. Wala hakusema tena, lakini aliendelea kumwangalia. Ndipo ule usiku kabla ya kuondoka... Alitakiwa kuondoka kesho yake asubuhi. Walikuwa wakifanya karamu nyingine kubwa. Naye akamtafuta. Hakuweza kumwona. Alijua

ilimbidi aoshe vyombo na kadhalika, kwa hiyo, kazi chafu na yote yangeweza kumwagwa nje.

¹⁴⁵ Basi hivyo ndivyo Kanisa la kweli la Mungu linapaswa kufanya wakati mwingine, kazi chafu, majina yote ya kashfa, na mambo yote yaliyo duni, kutupwa Kwake. Naye ni ndege mkubwa mwenye madoadoa. Ndege wengine wote hukusanyika na kukutanika Kwake. Hiyo ni sawa. Jina Lake liko kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo. Atatandaza bawa Lake kubwa siku moja apate kuruka. Yuko tayari. Hayo madoadoa yalimaanisha Damu ya Kristo aliyonyunyiziwa. Mnaona? Umelisoma katika Kitabu chako, Biblia.

¹⁴⁶ Basi mvulana huyu akampata maskini huyu msichana mdogo usiku huo akitoka nje. Akasema, “Nimekuchunguza. Hakuna ajuaye ila mimi mwenyewe.” Akasema, “Nimekuja huku kutafuta mke. Na katika wote niliopata kuona, umetimiza matakwa.” Alijisikiaje? Mtoto wa yule mtu mkubwa akimuuliza sasa kama angekuwa mkewe.

¹⁴⁷ Hebu wazieni tu jinsi wasichana hao hapana shaka walijisikia walipoangalia nje ya dirisha lao na kuona, ameshikana mikono, na maskini yule binamu, aliyedharauliwa, mtu ambaye walijaribu kumfanyia ubembe, pamoja na magauni yao yote makubwa na mapambo, wakipiga makelele.

Naye akasema, “Utakubali nikuo?”

“Loo,” akasema, “bwana, mimi sistahili.”

¹⁴⁸ Hivyo ndivyo Kanisa la kweli linavyojisikia kuhusu hilo, “Sistahili. Naweza...Kama ningeviosha tu vyombo vyako, itakuwa ni sawa.” Je, uko tayari kuchukua mahali hapo? Unaweza kuosha vyombo vya Chakula cha jioni? Je, uko tayari kuitwa mlokole? Au, uko tayari kushika njia pamoja na wachache wa Bwana waliodharauliwa? Je, uko tayari?

¹⁴⁹ Je, uko tayari, kazini mwako, kutiwa alama, “Kuna mtu, yeye ni shupavu wa dini, kwa sababu hatakunywa vileo, hatavuta sigara, hachezi dansi, hazururi na wanawake”? “Yule pale mwanamke ambaye anaweka kichwa chake chini, anatembea kama...kushuka kupitia mjini. Yeye si...Hatajiunga na makundi yetu”?

¹⁵⁰ Je, uko tayari kushika njia, kujiweka tayari kwa ajili ya Kuja kwa Bwana? Ikiwa unayo...Ukifanya hivyo, utakuwa unamngojea Yeye aje. Utafurahia Kuja Kwake. Halitakuwa jambo la kutisha. Utakuwa ni wakati wa neema sana unaoweza kufikiria, Kuja kwa Bwana. “Wale wote wanaopenda kuonekana Kwake.”

¹⁵¹ Kwa hiyo, alipoondoka, alimwambia kwamba angerudi wakati fulani. Kasema, “Utakapoanza kuona...” Ilikuwa majira ya baridi kali. Kasema, “Utakapoanza kuona miti hiyo ikianza kuchipua, kule, vichaka hivyo na kadhalika vikianza

kuchukua maisha mapya,” akasema, “basi nitarudi yapata majira ya kuchipua.”

¹⁵² Ninasikia, nisingeweza kusema ni kweli, lakini huyo msichana alipata tu dola moja na senti sabini na tano kwa juma kwa kazi yake. Lakini aliweka kila senti yake. Kwa nini? Alikuwa akijiandaa kwa ajili ya arusi ijayo. Aliweka akiba pesa zake kwa ajili ya gauni lake la arusi. Kwa maana yeye alisema, “Tutafunga ndoa papa hapa kwenye ranchi nitakapokuja tena.” Aliweka akiba pesa zake mwaka mzima. Alikuwa na furaha. Hakujali kuosha vyombo. Hakujali kupiga nguo pasi, wala kufagia nyumba ya wafanyakazi, wala chochote kile. Alikuwa ameposwa na bosi wa shamba hilo.

¹⁵³ Tunajali nini kile ulimwengu unachosema, Mkristo halisi? Tunajali nini kama ikitubidi kudharauliwa na kukataliwa? “Heri wenye upole, maana hao watairithi nchi.” Mwana wa Bosi anakuja, siku moja, na tutaenda kwenye Karamu ya Arusi. Je, inaleta tofauti gani kwetu, ikiwa unapenda kuonekana Kwake?

¹⁵⁴ Baada ya yote... Siku zikapita. Maskini wale mabinti, wale binamu, walimdhihaki, wakacheza dansi wakimzunguka, na kufanya kila kitu kingine. “Vema,” kasema, “ewe maskini, mtoto mjinga! Hujui kama yeye... Mbona, alikuwa kama wanaume wengine wote. Alikuwa anakutania tu.”

¹⁵⁵ Lakini Mwana wa Mungu hatanii. “Mtu asipozaliwa mara ya pili, hatapata kamwe...” Sijali jinsi unavyoonekana mzuri, jinsi ulivyo mshiriki wa kanisa, kile wadhifa wako ulicho nchini. Unaweza kuwa mwanasiasa. Unaweza kuwa katika serikali ya shirikisho. Unaweza kuwa katika Katoliki, Presbiteri, kanisa lolote unalotaka kuwa. Lakini, ni, “Mtu asipozaliwa mara ya pili, hutaingia. Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Ninanukuu tu Neno Lake.

¹⁵⁶ Hatimaye, ile saa ilipowadia, akaanza kuona haya, machipukizi yakaanza kuchipuka mitini. Alijua angekuwepo huko wakati wowote. Naye alisema, “Nitajaribu kufika huko kwenye machweo tu, ili tufunge ndoa na kuondoka mara moja.” Basi kila jioni, kwenye machweo ya jua, wakati yeye—yeye angeenda na kuchukua, kujiweka tayari kabisa, kuvaa maskini vazi lake la arusi, na kungoja langoni.

¹⁵⁷ Ndipo maskini binamu hawa walikuja na kumcheka, na kumdhihaki, na kusema, “Ewe maskini mtoto mjinga, mpumbavu. Kuwazia kwamba m—mtu anayemiliki... Yeye ndiye Rais, hasa, wa kampuni, kwamba mvulana wake angeoa mwosha vyombo!”

¹⁵⁸ Alikuwa anatafuta tabia, sio nguo. Alikuwa na pesa za kutosha kununua nguo zote zilizohitajika.

¹⁵⁹ Mungu hajali vitu vikubwa vya kupendeza ulivyo navyo. Anamiliki kila kitu duniani. Kwa hiyo, Yeye anataka tabia. Anataka kitu ambacho ni halisi.

¹⁶⁰ Na kwa hiyo, hatimaye, jioni moja, alipokuwa amesimama pale, nao walikuwa wakicheka na kumdhihaki, na kumwambia alikuwa mjinga. Mara ghafla, walisikia kwato zikirukaruka. Nini kilichotokea? Kutoka kilimani bukubodi ikaja. Sasa, bukubodi ni mkokoteni mdogo, wazi juu, maarufu sana huko Magharibi. Na farasi wote wakapiga kelele na kadhalika, wakija. Kutoka kilimani, ukaja mkokoteni huu, nao ukasimama mbele ya lango. Naye akakimbia. Akasema, “Nilijua utakuja.”

Hilo litakuwa ni Kanisa siku moja.

¹⁶¹ Akajitupa mikononi mwake, akasema, “Mpenzi, nimekuwa na mtu niliyemweka katika ranchi hii tangu nilipoondoka hapa mwaka jana, ambaye ameniletea ripoti ya kila kitu ambacho umefanya.”

¹⁶² Mungu ana Mtu aliyewekwa kwenye maskani hii, asubuhi ya leo, Yeye anaitwa Roho Mtakatifu. Anajua siri za moyo wako. Anajua kila kitu ambacho umefanya, au kile unachowazia. Anamwambia Baba kila kitu unachofanya. Analeta na kurudisha ujumbe huku na huko.

¹⁶³ Akasema, “Naye ameniambia kuwa umesubiri, na umefanya kazi, nawe umeshughulika kwa subira, ukiningojea nje. Sasa, umekuwa mtumwa kwa muda mrefu, lakini sasa siku zako za utumwa zimekwisha. Nimekuja pamoja na mhudumu, papa hapa chini ya ufito huu wa waridi, umekuwa mke wangu.” Akambusu, akaweka pete ya arusi kidoleni mwake, na kumnyanyua akamweka kwenye huo mkokoteni, huku amemkumbatia. Ndipo akaondoka, kutafuta ikulu hii kubwa mpya kwenye Barabara ya Nje huko Chicago, mahali palipotengwa nchini, ambapo angeweza kuishi kama bibi-arusi wake.

¹⁶⁴ Kwa nini? Alikuwa tayari. Alikuwa ameishi na kuwa aina ya mwanamke ambaye alimtaka. Ilitendeka tu kwa ghafla.

¹⁶⁵ Na huko Kuja ghafla kwa Bwana, kwa siri, ulimwengu haujui kutatukia, bali sisi tunajua. Kumekaribia. Usiwe kama maskini yule msichana waliyemvua nguo, katika Bandari ya Pearl, utaishia kwenye aibu. Kuwa kama Yule aliyeyiweka Mwenyewe tayari, na kuhifadhi maadili Yake, naye alikuwa akikungojea Kuja kwa Bwana, maana kutakuwa kwa siri na kwa ghafla.

¹⁶⁶ Mnapoyawazia mambo hayo, hebu na tumwinamishie vichwa vyetu Yeye Yule atakayekuja.

¹⁶⁷ Kabla tu hatujazungumza Naye, kila mwanamume kwa njia yake mwenyewe, kila mwanamke, mvulana, au msichana. Na wakati nikizungumza Naye na kujua ya kuwa Wakala Wake wa siri, Yule ambaye huwezi kumwona kwa jicho lako, kwa hiyo Yeye ni Wakala wa siri, Roho Mtakatifu aliyebarikiwa yuko humu jengoni. Je, ungetaka Yeye akukumbuke mbele ya Baba, asubuhi ya leo, kwamba unataka kuwa tayari, ndipo Yeye

atakapokuja, uende pamoja Naye? Kama ungetaka, je, waweza kumwinulia mkono wako? Bwana awabariki. Nadhani karibu kila mkono jengoni; wangu, pia. “Nataka Wewe, Roho Mtakatifu, umwambie Baba, ‘Inama uniangalie. Ni—ninashika njia pamoja na watu Wake waliodharauliwa. Na—nataka kwenda, nataka kuwa tayari. Na—nataka kuwa tayari sasa hivi, kwa sababu Yeye anaweza kuja kabla ibada haijaisha.”

Mataifa yanavunjika, Israeli inaamka,
Ishara walizotabiri manabii;
Siku za Mataifa zimehesabiwa, zimekumbwa
na hofu;
“Rudini, Enyi mliotawanyika, makwenu.”

Siku ya Ukombozi imekaribia,
Mioyo ya watu inavunjika kwa hofu;
Jazweni na Roho wa Mungu, taa zenu zikiwa
zimesafishwa na kuwa safi,
Tazameni juu! Ukombozi wenu umekaribia.
Mtini unakua; Israeli kurejeshwa.

¹⁶⁸ Ee Mungu! Mtini ukitoa machipukizi yake, Israeli wakirudi kama taifa! Nilipomsikia mchungaji wetu asubuhi ya leo, akisema, tuiombee Israeli! Hivi hamjui huko ndiko kuchipuza majani? Anapaswa kuja wakati huo.

¹⁶⁹ Nikiona hizo *Dakika Tatu Kabla Ya Usiku Wa Manane*, makala hayo, kuyaona kwenye—kwenye kamera yangu mwenyewe, au projekta kwenye chumba changu cha chini, wakati maskini wale Wayahudi walemavu na wakiingia kwa meli na kadhalika, kutoka kote ulimwenguni. Anayehoji alisema, “Je, mnakuja kwenye nchi ya uenyeji wenu, kufa katika nchi ya uenyeji wenu?” Akasema, “Hapana. Tumekuja kumwona Masihi.”

¹⁷⁰ Mtini unakua. Hivi hamwezi kuuona? Siku ya Ukombozi imekaribia.

Manabii wa uongo wanadanganya, Ukweli wa
Mungu wanaukana,
Ya kwamba Yesu aliye Kristo ndiye Mungu
wetu;

Hivi hamwezi kuona mahali tulipo?

Lakini tutatembea pale ambapo mitume
wamekanyaga.

Siku ya Ukombozi imekaribia,
Mioyo ya watu inazimia kwa hofu; (Wazia
jambo hilo!)
Jazweni na Roho wa Mungu, taa zenu zikiwa
zimetengenezwa na safi,
Angalieni juu! Ukombozi wenu umekaribia.

¹⁷¹ Bwana Mungu, katika wakati huu mkuu, ambapo ninaangalia kusanyiko hili dogo na kuona nyuso nyekundu na mashavu yenye madoa ya machozi, tunafahamu kwamba Wakala mkuu wa siri amesimama karibu, Roho Mtakatifu.

¹⁷² Sasa jalia tushike njia na wachache wa Bwana waliodharauliwa. Iwapo kuna aibu kidogo katika ujirani wetu, miongoni mwa watu, miongoni mwa kanisa, ama popote pale, hiyo haina uhusiano wowote nasi. Hatutachafua mavazi yetu kwa vitu vya dunia, tena. Kwa maana Wewe utakuja siku moja katika dakika moja, kufumba na kufumbua jicho, ule Unyakuo wa ghafla wa Kanisa Lako, wa siri. Utakuja kupitia kwenye kilima cha wakati, ushuke chini kwa upindo mlalo wa mvua, kulichukua Kanisa, kwa maana Maandiko yalisema, “Parapanda ya Mungu italia. Nao waliokufa katika Kristo watafufuka. Nasi tutanyakuliwa pamoja nao, hewani, kumlaki Bwana, na kuwa pamoja na Bwana milele. Kwa hiyo, ndugu zangu, farijianeni kwa maneno haya.”

¹⁷³ Hebu hilo lisikike kwenye kilindi cha mioyo ya kusanyiko hili asubuhi ya leo. Tutakusifu Wewe katika Jina la Yesu. Amina.



KUONDOKA GHAFLA KWA KANISA, KWA SIRI SWA58-1012

(The Sudden, Secret Going Away Of The Church)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza Jumapili asubuhi, tarebe 12 Oktoba, 1958, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2022 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org